

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA  
(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



Unapojibu tafadhali taja;  
Kumb. Na CDC/T20/2V0L1 /50

14/02/2023

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA UDEREVA ZA KUJITOLEA.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba anakaribisha maombi ya kazi za kujitolea kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi ya udereva.

**1. DEREVA II - NAFASI 7**

**1.0 SIFA ZA MUOMBAJI**

- I. Awe amehitimu kidato cha IV na kufaulu
- II. Awe na leseni daraja C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- III. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

**2. MAJUKUMU:**

1. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
  2. Kuhakikisha gari na vyombo vyake viko katika hali nzuri wakati wote, na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
  3. Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari
  4. Kutunza na kuandika daftari la safari "Log-book" kwa safari zote.
-


## **A. MASHARTI YA JUMLA**

1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania
2. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
3. Waombaji wawasilishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V.) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu wa kuaminika
4. Waombaji wote waambatishe nakala ya vyeti halisi na taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (passport size) ziandikwe jina la mwombaji nyuma
5. Testimonials Provisional results "Statement of results" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita HAVITAKUBALIWA
6. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za Kisheria.
7. Maombi yaandikwe kwa mkono na yatumwe kwa njia ya Posta kupitia anwani tajwa hapo chini.

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S.L.P.830,  
**CHEMBA.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 28/02/2023 saa 9.30 mchana.

Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri ya Chemba:[www.chembadc.go.tz](http://www.chembadc.go.tz)

  
Siwema H. Jumaa  
Mkurugenzi Mtendaji (W)  
**CHEMBA**  
MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
**CHEMBA**

---